



Amira Msellem Said ni msaidizi wake Sheikh Nabhany. Yeye pia ni mzaliwa wa Lamu na mwandishi wa mashairi, nyimbo, na riwaya. Ameshiriki katika jopo mbalimbali kuhusu lugha na utamaduni wa waswahili, hasa katika RISSEA, Mombasa.

Sheikh Ahmed Nabhany (OGW) alizaliwa Amu (Lamu) kisiwani mwaka 1927. Ni mshairi na msomi wa Kiswahili maarufu ulimwenguni. Walimu wake Sheikh Abdalla Bakathiri (Kadara), na Sheikh Bwanarehema Faraj wa Pate walimpa cheo cha Shaha, yaani bingwa wa tungo za Kiswahili. Nyanya yake Bi Amina Abubakar Sheikh alikuwa Shaha, na mwalimu wake pia. Sheikh Nabhany ni gwiji wa lugha, mila na desturi za waswahili. Amechangia katika halmashauri za lugha nchini Kenya na Tanzania, na ametambuliwa na vyuo vikuu na hata serikali kwa sababu ya kazi zake. Aendelea kufunza vizazi vya waswahili, na wasomi kutoka nchi za Ulaya na Amerika ambako amealikwa na vyuo mbalimbali mara kadhaa. Sheikh Nabhany ni Msaidizi wa Utafiti wa Mambo ya Ulimbe (Assistant Research Scientist) wa Taasisi ya Uchunguzi wa Waswahili ya Mashariki mwa Afrika (TUSIMA), ijulikanayo pia kama Research Institute of Swahili Studies of Eastern Africa (RISSEA).

JC Press

ISBN 978-0-9543960-3-9 90000

9 780954 396039

Waswifu wa Ahmed Sheikh Nabhany

Amira Msellem Said

Waswifu wa Ahmed Sheikh Nabhany



Amira Msellem Said

JC Press